



WIZARA YA UTAMADUNI, SANA  
NA MICHEZO

COSOTA  
COPYRIGHT SOCIETY OF TANZANIA

## TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA

### TAARIFA KWA UMMA

#### KUINGIA MABAKUBALIANO NA KAMPUNI YA SUMAJKT AUCTION MART LTD KUSAUDIA KUKUSANYA MIRABAHA

**Dar es Salaam - Aprili 13, 2022:**

Taasisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) imeanzishwa na Sheria namba 7 ya mwaka 1999 katika kifungu cha 46 Pamoja na kifungu cha 47 kimeipa COSOTA jukumu la kutetea na kulinda masilahi ya wabunifu nchini pamoja na kukusanya na kugawa mirabaha kwa wasanii kulingana na matumizi ya kazi zao katika maeneo ya biashara.

Na leo tarehe 13-04-2022 COSOTA kwa kutumia Mamlaka iliyopewa chini ya Kifungu cha 46 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki imeingia mkataba na Kampuni ya SUMA JKT Auction Mart Ltd kwa ajili ya ukusanyaji wa mirabaha katika Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma ambapo mkataba huu unaanza kazi mara moja,. kwa Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro tayari kuna Wakala anaendelea na kazi kwa niaba ya COSOTA aitwaye Tanzania Finance Corporation.

Ikumbukwe kwamba ni kosa la jinai kwa mtumiaji yoyote wa kazi za Sanaa katika maeneo mbalimbali ya biashara kutumia kazi hizo bila kulipia matumizi ya kazi hizo COSOTA au kupata kibali kutoka kwa msanii mwenyewe, adhabu yake ni faini isiyopungua kiasi cha Tsh 20,000,000 (Milioni ishirini) au Kifungo kisichozidi Miaka 3 au vyote kwa pamoja na adhabu hii ni kwa mujibu wa Sheria chini ya Hakimiliki na kifungu cha 42 cha sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki.

Utaratibu wa kukusanya na kugawa mirabaha umekuwa ukifanyika sehemu mbalimbali duniani na katika maeneo mbalimbali ya biashara yanayotumia kazi za Muziki na Filamu kama vile Baa, Hoteli, Kumbi za Sherehe, Kumbi za Starehe, Maduka makubwa, Vyombo vya Usafiri, Migahawa na kadhalika.

Katika kuhakikisha COSOTA inatekeleza adhima ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha Wasanii wananaufaika na matumizi ya kazi zao katika maeneo mbali mbali ya kibashara COSOTA inaendelea kuingia mikataba na mawakala katika sehemu mbalimbali ili kuhakikisha inaongeza makusanyo kwa kufikia maeneo mengi nchini.



WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA  
NA MICHEZO

COSOTA  
COPYRIGHT SOCIETY OF TANZANIA

TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA

Aidha, COSOTA inaomba mawakala hawa kupewa ushirikiano kule kote watakapopita na Mawakala hao watatambulika kwa vitambulisho vilivyotolewa na COSOTA pamoja kwa upande wa mawakala kutoka SUMAJKT watatambuliwa kwa vitambulisho vy'a ofisi yao.

Wito kwa watumiaji wote wa kazi za Muziki na Filamu nchini katika maeneo ya biashara kuhakikisha wanalipia matumizi ya kazi hizo COSOTA ili kuepusha usumbufu pale zoezi la operesheni ya ukaguzi litakapofanyika.

Imetolewa na :

Philemon Kilaka

**KAIMU AFISA MTENDAJI MKUU NA  
MSIMAMIZI WA HAKIMILIKI**